

Vigezo na Masharti:

1. Nani anaweza kushiriki

Ili kushiriki shindano, mteja anatakiwa kuwa na umri usiopungua miaka 18, awe na simu ya mkononi yenye namba ya simu anayoimiliki kwa mujibu wa sheria na taratibu za huduma za mawasiliano nchini Tanzania.

2. Nani hawezi kushiriki

Wakurugenzi, wafanyakazi na wanafamilia wao hawataruhusiwa kushiriki kwenye shindano na hawatakuwa na sifa za kupewa zawadi yoyote katika shindano hili.

3. Muda wa Shindano

Shindano litaanza tarehe 14 Septemba, 2018 na kuisha usiku wa tarehe 17 Januari, 2019. Hata hivyo, kwa kuzingatia sheria, muda wa shindano, unaweza kuongezwa au kupunguzwa kwa kadri muendeshaji atakavyoona inafaa.

4. Jinsi ya kushiriki

- Unapo piga (*150*62#) moja kwa moja unakuwa umefanya usajili wa awali wa akaunti yako ya CRDB-SimAccount. Baada ya hapo, utapewa nafasi ya kukamilisha usajili kwa kutembelea mawakala wa FAHARI HUDUMA na matawi ya Benki ya CRDB yaliyosambaa nchi nzima. Usajili KAMILI wa akaunti yako ya SimAccount, utakupa nafasi ya moja kwa moja kuingia kwenye shindano.
- Matumizi yoyote mengine ya huduma za SimAccount, kama vile kuweka fedha, kuhamisha fedha, kulipia Bili na bidhaa, yatakuongezea nafasi za kushinda. Utakapofanya matumizi hayo ya huduma za SimAccount, utapokea ujumbe mfupi kuthibitisha muamala uliufanya.

5. Gharama za kushiriki shindano

- Hakuna gharama kwenye upande wa SimAccount ili kushiriki shindano hili. Gharama pekee ambazo mteja anaweza kuingia ni zile tu zinazohusiana na huduma za miamala ya SimAccount. Mfano kulipa LUKU, kununua bidhaa dukani kwa SimAccount nk.
- Shindano hili liko kwenye 'Huduma ya haraka ya mawasiliano inayotumiwa na simu za mkononi kuwasiliana na watoa huduma wa mitandao (USSD)', hivyo kunaweza kuwa na gharama kutoka kwenye mitandao husika ya simu.

6. Droo na zawadi

1. Zawadi za kila siku

- Hadi Tsh 20,000/- kushindaniwa ambayo itawekwa kwenye SimAccount ya Mshindi
 - Kila saa - TSH 5000/-
 - Pambazuka -TSH 20,000/-
 - Lala Salama -TSH 20,000/-
- Idadi ya chini ya washindi ni 2800

2. Zawadi za kila wiki

- Hadi Tsh 2,000,000/- kushindaniwa ambayo itawekwa kwenye SimAccount ya Mshindi
 - Zali - washindi kumi kila mmoja TSH 100,000/-
 - Kabambe - mshindi mmoja TSH 1,000,000/-
 - Bingwa - mshindi mmoja TSH 2,000,000/-
- Idadi ya chini ya washindi ni 1060

3. Zawadi za kila mwezi

- Hadi Tsh 10,000,000/-kushindaniwa ambayo itawekwa kwenye SimAccount ya Mshindi
 - WOW - mshindi mmoja TSH 1,000,000/-
 - Mzuka - mshindi mmoja TSH 5,000,000/-
 - Kitita - mshindi mmoja TSH 10,000,000/-
- Idadi ya washindi ni 3

4. Funga dimba

- Hadi milioni Tsh 20,000,000/-kushindaniwa ambayo itawekwa kwenye SimAccount ya Mshindi

Kwa maelezo Zaidi tembelea tovuti yetu www.simaccount.co.tz / +255 755 19 77 00